



## Mamlaka ya Makazi ya Jiji la Austin Onyesho la Mradi wa Usaidizi wa Ukodishaji(RAD) Maelezo ya Jumla

---

Mamlaka ya Makazi ya Jiji la Austin (HACA) iko mtari wa mbele kupitia mkakati wake mpya jasiri ili kulinda makazi ya umma jijini Austin na kuimarisha maisha ya zaidi ya wakazi wake ambao ni zaidi ya 4,300 na wanaotegemea makazi ya umma.

Kwa kushiriki katika mpango mpya wa Idara ya Makazi na Maendeleo ya Mjini nchini Marekani (HUD) maarufu kama Onyesho la Msaada wa Ukodishaji (RAD), HACA itaweza kufadhili maboresho muhimu yanayohitajika sana kwa nyumba zake nzee na kuhakikishia wakazi wake wenye mapato ya chini kwamba nyumba hizo zinapatikana kwa miaka 40 ijayo. RAD itatafuta fursa zaidi ili wakazi wake wawe na uwezo wa kuchagua nyumba siku za usoni.

### Muhtasari wa RAD

RAD ilianzishwa na HUD ili kushughulikia ukarabati na uboreshaji wa nyumba zenye malibikizi ya thamani ya dola bilioni 26. Chini ya Mpango wa RAD, ruzuku ya nyumba zilizopo sasa (na zinazoendelea kukosa dhamana) hubadilishwa na kuwa mikataba ya usaidizi wa kodi kwa kila nyumba. Kufanya hivyo mamlaka za makazi zinapata nafasi ya kufadhili ukarabati na utunzaji wa nyumba za makazi ya umma zinazozeeka.

### Umuhimu wa RAD kwa Wakazi

- **Ulinzi:** Kila mkazi ana haki ya kuishi katika nyumba ya umma na kurudi kwenye nyumba iliyoboreshwa katika nyumba yake ya awali. Bado kodi itasalia kuwa asilimia 30ya makadirio ya pato la familia nzima, na hakuna mtu atahitaji kuchunguzwa upya ili athibitishwe kuwa anastahiki. HACA itadumisha huduma za hali ya juu kwa wakazi wake.
- **Uboreshaji.** Nyumba nyingi zitafanyiwa uboreshaji unaohitajika, na nyumba nyingi zitaboreshwa ipasavyo, zitafanywa kuwa za kisasa, na kuwa zenye matumizi mazuri ya nishati. Wakazi watakuwa na haki ya kutoa maoni yao kuhusu uboreshaji huu ili kuhakikisha kwamba shughuli hii inakidhi mahitaji yao.
- **Uchaguzi.** Siku za usoni, wakazi wa sasa na wanaotuma maombi kwa mara ya kwanza wataweza kutuma maombi na kuishi katika nyumba mahsusi wanazochagua, badala ya kupewa nyumba ambayo inapatikana ya kwanza. Wakazi watakaosalia katika mojawapo ya nyumba za RAD kwa muda wa miaka miwili wataweza kutuma maombi wakitumia Vocha ya Kuchagua Nyumba ambazo zitawaruhusu kutafuta nyumba katika soko la nyumba za kukodi za kibinafsi.

### Pata Maelezo Zaidi Kuhusu RAD

Kama wewe ni mkazi wa nyumba za umma za HACA na una maswali kuhusu namna mpango wa RAD utakavyokuathiri wewe na familia yako, tafadhali piga kwa nambari ya simu inayopatiakana kila wakati ya RAD kupitia 1-(844) HACA-RAD (422-2723) au tutumie barua pepe kupitia [hacarad@hacanet.org](mailto:hacarad@hacanet.org). Unaweza kupata maelezo zaidi, pamoja na Maswali Yanayoulizwa Sana mtandaoni katika [www.hacarad.org](http://www.hacarad.org).